# MAPENZI YAKE YATIMIZWE

**Na Jacquelyn Fedor**

**Ilitafsiriwa Na David Odhiambo**

**Wakolosai 1:16-17**

16 Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana, ikiwa ni viti vya enzi au utawala au wakuu au mamlaka. Vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake.

17 Naye alikuwako kabla ya vitu vyote, na **katika Yeye vitu vyote huungana**.

Kwa hivyo tukumbuke, katika Yeye vitu vyote huungana.

Sasa hebu tusome **Waefeso 1:10**

10 kwamba katika wakati mkamilifu wa nyakati apate kuvikusanya **kuwa moja** vitu vyote **katika Kristo**, vilivyo mbinguni na vilivyo duniani—**katika Yeye**.

Sasa unaona kwamba atavikusanya vitu vyote mbinguni na duniani (ndani yake)? Ninachotaka kuonyesha kupitia ujumbe huu, ni kwamba vitu vyote, mwishowe, vitakuwa kimoja katika Kristo. Shetani anaelewa kwamba ikiwa hili litatimizwa, ndoto zake zote za ukuu zitatoweka kama moshi. Jambo

moja ambalo linaweza kumhakikishia muda zaidi wa kutimiza amri zake katika Isaya 14, ni kuweka vitu vyote vimegawanyika. Kwa kuwa vitu vyote viliumbwa na Kristo, ulimwengu wote ndio lengo lake, kwa hivyo atafanya awezavyo kuleta mgawanyiko kwa kila njia inayowezekana. Kwa mfano, sheria za mbinguni zilivunjwa alipowatambulisha binti za wanadamu kwa malaika wa mbinguni, na kusababisha kuvuka kwa spishi. Alimdanganya Hawa, na kumfanya achague maarifa yake badala ya Neno. Hii iligawanya Ufalme wa Mungu tangu kuanzishwa kwake hapa duniani. Adamu na Hawa sasa walikuwa wamekusudiwa kuishi maisha yao kupitia kiumbe huyu ambaye alikuwa amejitolea kuona vitu vyote vimegawanyika ili aweze kuvitawala. Hivyo dunia iligawanywa katika nchi, kaunti, miji, mataifa, serikali n.k. Wale waliozaliwa katika ulimwengu wake waliyakubali yote kama kawaida. Lakini, kama tulivyoona katika Waefeso 1:10, mwishowe vitu vyote vitakusanywa pamoja kama kitu kimoja katika Yeye. Pia, kama tulivyoona katika Wakolosai 1:16-17, vitu vyote vinajumuishwa katika Yeye, au vitu vyote vinaendelezwa na Yeye. Kila kitu ni sehemu yake. Kwa maneno mengine, Kristo ndiye kiini cha vitu vyote, vitu vyote viliumbwa kutoka kwa sehemu yake. Kwa hivyo, vitu vyote vinahusiana kwa njia moja au nyingine ili kuwa kitu kizima, au kuwa kitu kimoja.

Katika Mwanzo tunamwona Baba akizungumza na Mwanawe, akimwambia amuumbe mwanadamu kwa mfano wao, kwa mfano wao. Alimuumba mwanadamu kutoka sehemu ya sayari na akapuliza pumzi yake ndani ya

mwanadamu, tena akimfanya kuwa sehemu yake. Hii ina maana kila kitu alichokiumba baada ya hapo, au kile kilichoumbwa hata kabla ya Adamu ilikuwa sehemu Yake. Tena, ninajaribu kuonyesha kwamba vitu vyote ni sehemu ya kitu kizima, au sehemu ya Kristo. Kwa mfano, tunaona ambapo Baba alimwomba Yesu atengeneze nuru ambayo ingeleta uzima na mwanga kwenye sayari yetu wakati wa mchana, na mwangaza kutoka kwa nuru hiyo uliunda mwezi ambao ungetoa mwanga wakati wa usiku. Nuru hiyo ilitoka kwa Yesu. Sasa hebu tuangalie Yohana ambapo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Baba yuko ndani yangu, mimi niko ndani yake nasi tuko ndani yenu.

**Yohana 14:20**

20 Siku hiyo mtajua ya kuwa **mimi** niko **ndani ya Baba yangu**, **nanyi** ndani **yangu**, **nami** ndani **yenu**.

Kwa hivyo je, mnaweza kuona uhusiano wetu na Muumba wa vitu vyote, na kutufanya tuhusiane na vitu vingine vyote vilivyoumbwa pia, sehemu ya kitu kizima, au kitu kimoja na vitu vyote? Baba aliona haya yote yakitokea na Shetani na jozi ya kwanza kabla hayajawa ukweli na akapanga mpango wa kurejesha vitu vyote kwake mwenyewe licha ya amri za Shetani kwamba angechukua nafasi Yake ya ukuu. Mpango huu ulifanywa uonekane kwa urahisi duniani. Mwanadamu na viumbe vyote, akiwemo Shetani, waliweza kuiona tu walipotazama juu mbinguni.

**Zaburi 19:1-6** inatufunulia hili.
1 **Mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu**; na **anga** inaonyesha **kazi ya mikono Yake**.
2 **Mchana** kwa **mchana** hutamka **maneno**, na **usiku** kwa **usiku** hufunua **maarifa** (ujumbe wa urejesho na ushindi wa Kristo
uko angani).
3 Hakuna usemi wala lugha ambapo sauti yao haisikiki.
4 Kauli yao imeenea **duniani kote**, na **maneno yao** hadi **mwisho wa dunia**.
Ndani yao ameweka **hema kwa ajili ya jua**,
5 Ambayo ni kama **bwana harusi** akitoka **chumbani mwake**, na hufurahi
kama mtu mwenye nguvu **ili kukimbia mbio zake**.
6 Kuinuka kwake ni **kutoka mwisho mmoja wa mbingu**, na mzunguko
wake hadi **mwisho mwingine**; na **hakuna kitu kilichofichwa** kutokana na
**joto lake**.

Kwa hivyo kuna mchoro wa mpango wa Mungu wa urejesho ambao ni mlango wa ushindi kwa wanadamu ambao hakuna kinachoweza kubadilika, hakuna kinachoweza kushinda na Bwana pekee ndiye anayeshikilia ufunguo. Yote yako kwenye nyota. Tunaposoma mistari ya 7-11 ya Zaburi 19, tutapata mwanga wa kile tunachopaswa kufanya ili kuunganisha mgawanyiko wa sayari yetu na ulimwengu na kufanya tena uumbaji kuwa mmoja na Muumba wake. Kwa hivyo hebu tuchambue maandiko haya ili kutupa kidokezo cha jinsi ya kupata ushindi.

**Zaburi 19:7a**

7 Sheria ya Bwana ni kamilifu, inabadilisha roho (utii kwa sheria ya Mungu utabadilisha roho yetu wa nje ambaye Shetani amemwumba kwa mfano wake);

Kwa urahisi wa kuelewa Mungu aliandika sheria zake mioyoni mwetu na akilini mwetu.

**Waebrania 8:10**

10 Kwa maana hili ndilo **agano nitakalofanya** na **nyumba ya Israeli** baada ya siku zile, asema Bwana: **Nitaweka sheria zangu** katika **akili zao,** na kuziandika **mioyoni mwao**; **nami** nitakuwa **Mungu** wao, **nao** watakuwa **watu wangu**.

**Zaburi 19:7b**

Ushuhuda wa Bwana ni hakika, humtia wanyonge hekima;

Kwa maana yeye aaminiye ana uhakika wa matokeo kamili, kama vile Neno lilivyo kamili.

**Malaki 3:6**

6 "Kwa maana mimi ni Bwana, **sibadiliki**; kwa hiyo hamjaangamizwa, enyi

wana wa Yakobo.

**Waebrania 13:8**

8 Yesu Kristo ni **yeye yule jana, leo**, na **hata milele** (kamili).

**Zaburi 19:8a**

8 Amri za Bwana ni za haki, hufurahisha moyo;

Mungu ni mkamilifu, kwa hivyo sheria zake ni kamilifu, na kama tungezitii tu, kuzifuata kama ramani ya kuishi, sisi pia tunaweza kuwa wakamilifu. Sababu ya sisi kunaswa katika ulimwengu wa Shetani leo, tukiwa tumetekwa na mifumo yake, ni kwa sababu Adamu na Hawa hawakutii. Tukifuata historia ya mwanadamu katika vizazi vyote, tutaona kwamba walikuwa wamepotoka na Mungu kila mara kwa sababu ya kutotii kwao. Kama mfano hebu tuangalie Yeremia 7.

**Yeremia 7:22-24**

22 Kwa maana sikusema na baba zenu, wala sikuwaamuru siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri, kuhusu sadaka za kuteketezwa au dhabihu.

23 Lakini hili ndilo nililowaamuru, nikisema, '**Tiini sauti yangu**, nami **nitakuwa Mungu wenu**, **nanyi** mtakuwa **watu wangu**. **Mkaende** katika **njia zote nilizowaamuru**, **mpate kufanikiwa**.'

24 Lakini **hawakutii** wala hawakutega sikio lao, bali **walifuata** **mashauri**
na **ukaidi** wa **mioyo yao mibaya**, **wakarudi nyuma** wala si mbele.

**Kumbukumbu la Torati 28:1**

1 "Sasa **itakuwa**, **ukiitii sauti ya Bwana Mungu wako kwa bidii**, na
**kuzishika amri zake zote** ninazokuamuru leo, ndipo **Bwana Mungu wako**,
atakuweka **juu ya mataifa** yote ya **dunia**.

Mungu amekuwa akimwambia mwanadamu katika vizazi vyote, kwamba tukisikia sauti yake na kutii, tutabarikiwa, mambo yangeweza kugeuzwa.

Hebu tuangalie **Luka 11:28.**

28 Lakini akasema, "Zaidi ya hayo, **heri wasikiao neno la Mungu** na
**kulishika**!"

**Zaburi 19:8b**

**Amri ya Bwana** ni **safi**, **huyatia macho nuru**;

**1 Yohana 3:21-22**

21 Wapenzi, mioyo yetu isipotuhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu.
22 Na chochote tunachoomba tunapokea kutoka kwake, **kwa sababu**
**tunazishika amri zake** na **kufanya** **mambo** yanayo **mpendeza**
**machoni pake**.

Kwa hivyo kama tunavyoweza kuona, tukifuata sheria, itatuongoza katika juhudi zetu za kutembea katika njia ya ushindi. Ezekieli alitabiri jambo hili maelfu ya miaka iliyopita.

**Ezekieli 20:19-20**

19 **Mimi** ndimi **Bwana Mungu wenu**: **Enendeni katika amri zangu**,
**mshike hukumu** zangu,na **kuzifanya**;
20 **takatifu Sabato zangu**, **nazo** zitakuwa **ishara** kati **yangu na ninyi**,
mpate **kujua** ya kuwa **mimi ndimi Bwana Mungu wenu**.'

Yesu alisema katika **Yohana 15:10**,

10 **Mkizishika amri zangu**, **mtakaa katika upendo wangu**, kama vile mimi
**nilivyozishika amri za Baba yangu** na **kukaa katika upendo wake**.

Kwa kweli Neno linatuambia tukimpenda Mungu tutazishika amri zake, hivyo kutotii kwetu, mtazamo wetu wa kidunia wa "Ninafanya kwa njia yangu" umesababisha ulimwengu tunaoishi leo.

**Zaburi 19:9a**

9 **Kumcha Bwana** ni **safi**, hudumu milele;

Labda hii ndiyo sababu kuna uasi mwingi leo, kuna hofu kidogo au hakuna

kabisa ya Mungu. Neno hilo hofu linaweza kumaanisha tu kumcha Mungu, lakini wakati huo huo tunaweza kuona wazi kwamba kutotii kwetu, ukosefu wetu wa upendo kwa Neno na utii wake, kunaweza kusababisha kifo chetu. Mungu ni Mungu wa upendo. Lakini alimuumba mwanadamu kama sehemu ya familia yake kwa mfano wake, na inamkasirisha mwanadamu anapotembea kinyume na jinsi alivyoumbwa. Baba alisema katika Mwanzo 6 kwamba alijuta hata kwamba alimuumba mwanadamu, na kusababisha uharibifu tuliouona katika gharika ya Nuhu! Tazama alichofanya kwa Sodoma na Gomora, na jinsi maelfu ya Waisraeli walivyokufa katika Hesabu 25:6-9 kwa sababu ya kutotii kwa mwanamume mmoja kuchukua mwanamke kutoka miongoni mwa wapagani. Kwa hivyo tunaweza kuona tunaweza kufanya vizuri kutakasa jina la Mungu, kumheshimu Muumba wetu, kujiruhusu kukamilishwa na kurejeshwa kwenye ukamilifu wetu wa asili na kwa mfano wake. Sote tunaweza kutembea naye, au kufanya chaguo lile lile Adamu na Hawa walifanya, ambao ni wazi hawakuwa na hofu ya Mungu na kutembea na Shetani.

**Mithali 1:7**

7 **Kumcha** **Bwana** ni **chanzo cha maarifa**, Bali **wapumbavu** hudharau **hekima** **na** **mafundisho**.

**Mithali 9:10**

10 "**Kumcha** **Bwana** ni **mwanzo wa hekima**, na **maarifa** ya **mtakatifu** ni

**ufahamu**.

**Zaburi 33:8**

8 **Dunia yote na imche Bwana**; **wote wakaao duniani na wamche**.

Kuna wale ambao wangesema kwamba huyo ni Mungu wa Agano la Kale, lakini kama tulivyosema hapo awali, Mungu habadiliki, na Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele!

**Mathayo 10:28**

28 Wala msiwaogope wale wauao mwili lakini hawawezi kuua roho; bali **mmwogopeni yeye** awezaye **kuangamiza roho** na **mwili kuzimu**.

Je, unaweza kuona hitaji la kumjua Mungu vizuri zaidi, kuondoa akili na mioyo yetu maarifa tuliyoyapata kutoka katika ulimwengu huu na kukuza upendo kwa ujuzi wa Mungu? Tunawezaje kuwa na hofu au kumpenda Mungu ambaye hatumjui kwa undani na kama watoto wake, kuogopa kutotii sheria zake, kanuni zake, na njia zake?

**2 Wakorintho 7:1**

1 Kwa hiyo, wapenzi, tukiwa na ahadi hizi, na **tujitakase** na **uchafu wote wa mwili** na **roho**, tukikamilisha **utakatifu** katika **kumtii Mungu**.]

**Zaburi 19:9b**

**Hukumu** za **Bwana** ni za **kweli** na **za haki** kabisa.

Wanadamu leo wamezoea sana kufanya kazi kupitia akili zao kulingana na maarifa ya Shetani kiasi kwamba ni vigumu sana kwao kuelewa njia za Mungu haziwezi kupotoshwa, wala utu wake hauwezi kudhibitiwa. Yeye ni Mwamba wa ukamilifu, usiotikisika. Tunawezaje kutilia shaka hukumu zake? Kwa wale ambao wamezoea kuongozwa na maadili ya ulimwengu huu, inaweza kuwa vigumu kumwelewa Mungu huyu asiyebadilika, lakini kama Neno litakavyotuonyesha, Yeye ndiye Hakimu mkuu ambaye sote tutasimama mbele yake, si katika kivuli cha wake au waume, baba au mama au marafiki, bali peke yetu kabisa. Tutalazimika kutoa hoja ya mwenendo wetu tunaposimama mbele ya Muumba wa ulimwengu, hakimu anayeona mambo yote, anayejua mambo yote, anayesikia mawazo yetu. Tukipatikana miongoni mwa wasiotii, nakuahidi, siku hiyo, tutamwogopa na kutamani kama tungeshika amri zake!

**Warumi 14:10-12**

10 Lakini mbona unamhukumu ndugu yako? Au mbona unamdharau ndugu
yako? **Kwa maana sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo**.
11 Kwa maana imeandikwa: "**Kama niishivyo**, **asema Bwana**, **kila goti
litapigwa mbele zangu**, na **kila ulimi utakiri kwa Mungu**."
12 Basi **kila mmoja wetu atatoa hoja juu yake mwenyewe mbele** ya

**Mungu**.

**Ufunuo 20:12**

12 Nikawaona wafu, wadogo kwa wakubwa, **wamesimama mbele za Mungu**, na **vitabu vikafunguliwa**. Na **kitabu** **kingine** kikafunguliwa, ambacho ni **Kitabu cha Uzima**. Na **wafu wakahukumiwa kulingana na matendo yao**, **kwa** **mambo** **yaliyoandikwa katika vitabu**.

Kutimizwa kwa andiko hili kutakuwa kwa kutisha kwa wale wasiotii na waasi, lakini kwa wale wampendao na kuzishika amri zake, ni wakati wa kutisha kama nini, wa kutisha tu kwa maana ya kuwa wadogo sana mbele za Baba yetu, Muumba wetu! Je, wazo hili si sababu ya kutaka kukamilishwa na kubadilishwa kupitia utii wetu kwa amri zake? Tunaposikia na kutii, tunajidhihirisha zaidi kama watoto wa Mungu, wale ambao wamekuwa wafadhili wa karamu ya mwisho, Simchat Torah, ambayo inamaanisha kufurahi katika sheria.

Acha nifunge na andiko hili la mwisho,

**Zaburi 19:10-11**

10 **Zinazotamanika zaidi** (amri zake) kuliko **dhahabu**, naam, kuliko dhahabu safi nyingi; **tamu** kuliko **asali** na **sega ya** **asali**.
11 Zaidi ya hayo, mtumishi wako **anaonywa nazo**, na **katika kuzishika**

kuna **tuzo kubwa** (ukamilifu, urejesho).

Utii wetu kwa sheria za Mungu utaturudisha katika upatanisho na viumbe vingine vyote na Muumba wetu akitufanya sehemu ya yote tunapokusanyika ndani Yake. Ufalme Wake na uje na mapenzi yake yatimizwe. Sote tuwe sehemu ya yote!

Tembelea tovuti yetu http://www.trumpetsoftruth.com